# Ulega atoa siku 30 kukomesha uhalifu

Na ATHNATH MKIRAMWENI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega amemwagiza Mkurugenzi wa Uvuvi, Profesa Mohamed Sheikh kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha ndani ya mwezi mmoja wanakomesha vitendo vya uvuvi haramu katika ukanda wa Pwani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, jana, katika hafla ya ugawaji wa boti za kisasa kwa wavuvi wa mkoa Dar es Salaam, Ulega aliwaagiza wavuvi kushirikiana na viongozi wa serikali kutoa taarifa za watu wanaovua kwa kutumia milipuko.

Alisema boti hizo zimetolewa kwa mikopo chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), hivyo endapo wavuvi wataonekana ni waaminifu, wanaweza kupata fursa ya kukopeshwa nyingine.

"Tunajua mahitaji ya samaki ni makubwa lakini njia mnazotumia kuvua hamuwezi kupata mazao mengi zaidi, tayari zimeshaidhinishwa fedha nyingine kama sh. bilioni 11 kwa ununuzi wa boti nyingine," alisema.

Pia, aliwataka wavuvi hao kutumia boti hizo kujenga uchumi na familia zao badala ya kuendeleza malumbano katika vikundi vyao.

"Msiende kufanya kuwa chanzo cha mfarakano mkazitumie kuzalisha tutoke katika kuchangia asilimia 1.8 katika pato la taifa na tufike asilimia 10 mwaka 2030," alisema.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Riziki Shemdoe alisema utoaji wa boti hizo ni mkakati wa kuwawezesha wavuvi wadogo katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Alisema katika awamu ya kwanza jumla ya boti 160 zenye thamani ya sh. bilioni 11.5 zitatolewa kwa wanufaika nchi mzima.

Profesa Shemdoe alisema boti 92 zitatolewa katika ukanda wa Pwani na 27 kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

"Leo (jana) tutakabidhi boti 11 zenye thamani ya sh. milioni 798.75 ambazo zitakabidhiwa katika maeneo ya Bagamoyo, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Kibiti na maeneo mengine," alisema.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya Ilala, Edward Mpogolo alisema boti hizo zitasaidia kuimarisha uvuvi wilayani Ilala.

Mpogolo alisema bado wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto ya uvuvi haramu wa kutumia mabomu kuvua samaki, hivyo aliahidi kutekeleza maelekezo ya Waziri Ulega na kwamba anakwenda kupambana nao kutokomeza uvuvi huo kwa mkoa wa Dar es Salaam.

CamScanner

UHURU UK 7

# TANGAZO KWA UMMA

## MIKOPO YA PEMBEJEO ZA UFUGAJI SAMAKI KWA VIZIMBA AWAMU YA PILI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inakaribisha maombi ya mkopo wa masharti nafuu. Mkopo huo unalenga kutoa pembejeo za ufugaji samaki kwa vizimba kibiashara katika Ziwa Victoria. Mkopo utajumuisha vizimba vya mviringo vya plastiki na chuma vyenye kipenyo cha mita 6, 8 na 10; vifaranga vya samaki sato; na chakula cha samaki. Walengwa ni vyama vya ushirika/vikundi, makampuni na watu binafsi wanaokidhi vigezo.

Maombi yaambatanishwe na andiko la biashara pamoja na muhtasari wa kikao ulioridhia kukopa na ukomo wa madeni kwa vyama vya ushirika; barua ya dhamana kutoka halmashauri husika kwa vikundi; na dhamana ya mkopo kwa mtu binafsi na kampuni. Maelezo ya kina yanapatikana katika tovuti ya Wizara
**www.mifugouvuvi.go.tz**, Ofisi za Uvuvi Halmashauri husika na Ofisi za Wizara zinazoshughulika na masuala ya Uvuvi.

Maombi yote yaidhinishwe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na kutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kabla ya tarehe 29 Januari, 2024 kupitia anuani ifuatayo;


**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**
**S.L.P 2847**
**40487-DODOMA**
**Simu: +255 26 23 22613**
**Baruapepe: ps@uvuvi.go.tz**


CamScanner

# Uvuvi haramu wamchefua Waziri Ulega

Fortune Francis, Mwananchi
ffrancis@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ameagiza kuondolewa katika nafasi yake Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi, Stephen Lukanga kwa kushindwa kupanga na kutekeleza mikakati thabiti ya kukomesha uvuvi haramu.

Alitoa agizo hilo jana jijini hapa, alipokabidhi boti 11 zenye thamani ya Sh1.85 bilioni zilizotolewa kwa mkopo kwa wavuvi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akikata utepe ikiwa ni ishara ya kukabidhi boti kwa wavuvi wa Mkoa wa Dar es Salaam. **Picha na Said Khamis**

Waziri Ulega alifikia uamuzi huo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wadau wa uvuvi mkoani hapa kuhusu kukithiri kwa vitendo vya uvuvi haramu katika ukanda wa Pwani, hususan Dar es Salaam.

Oktoba 4, mwaka huu akiwa mkoani Mwanza katika soko la Lumumba, Ulega alimpa mwezi mmoja Lukanga kuhakikisha anapanga na kutekeleza mikakati ya kukomesha uvuvi haramu ambao umekuwa kikwazo kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi.

Waziri Ulega, aliagiza nafasi hiyo apewe aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani, Profesa Mohamed Sheikh ambaye alimuagiza ashirikiane na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha ndani ya mwezi mmoja vitendo hivyo vinakomeshwa.

Pia amemuagiza kuangalia idara moja baada ya nyingine kama maofisa uvuvi waliopo wanaweza kazi hiyo.

"Nimewasika wakuu wa wilaya wakizungumzia juu ya kadhia ya uvuvi haramu, tena uvuvi wa mabomu ukiwa umeenea katika pwani yetu, imekuwa ni kero kubwa. Nimefurahi viongozi wao wenyewe wameonyesha utayari wa kuhakikisha wanalisimamia jambo hili," alisema na kuongeza:

"Namuelekeza mbele ya hadhara hii na huyo tunakwenda kumpa kazi ajue jambo la kwanza ashirikiane na vyombo vingine vya Serikali, tunataka kuambiwa ndani ya mwezi mmoja hakuna bomu linapigwa ndani ya ukanda huu".

Akizungumzia ugawaji wa boti hizo, Ulega alisema walifikia hatua hiyo baada ya kuona mahitaji ya samaki ni makubwa, lakini upatikanaji wa wake ni mdogo kutokana na vifaa wanavyotumia kutokuwa na uwezo.

"Msiende kuzifanya kuwa chanzo cha mafarakano, mkazitumie boti hizi kuzalisha tutoke kwenye kuchangia asilimia 1.8 kwenye pato la Taifa tufike asilimia 10 itakapofika 2030," alisema.

Awali, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Riziki Shemdoe alisema utoaji wa boti hizo ni mpango wa kuwawezesha wavuvi wadogo katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo alisema changamoto kubwa wilayani humo ni uvuvi haramu wa kutumia zana zenye athari, yakiwemo mabomu.

Julai mwaka huu wakati wa mkutano wa Msajili wa Hazina na wahariri wa vyombo vya habari, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege alisema mikopo iliyotolewa kwa wavuvi ni utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu.

Alisema mikopo hiyo inatumiwa kwa ajili ya ununuzi wa boti za kisasa, ujenzi wa vizimba vya kufugia samaki, kuendesha kilimo cha mwani na kutoa ushauri wa kitaalamu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# TANGAZO KWA UMMA

## MIKOPO YA PEMBEJEO ZA UFUGAJI SAMAKI KWA VIZIMBA AWAMU YA PILI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inakaribisha maombi ya mkopo wa masharti nafuu. Mkopo huo unalenga kutoa pembejeo za ufugaji samaki kwa vizimba kibiashara katika Ziwa Victoria. Mkopo utajumuisha vizimba vya mviringo vya plastiki na chuma vyenye kipenyo cha mita 6, 8 na 10; vifaranga vya samaki sato; na chakula cha samaki. Walengwa ni vyama vya ushirika/vikundi, makampuni na watu binafsi wanaokidhi vigezo.

Maombi yaambatanishwe na andiko la biashara pamoja na muhtasari wa kikao ulioridhia kukopa na ukomo wa madeni kwa vyama vya ushirika; barua ya dhamana kutoka halmashauri husika kwa vikundi; na dhamana ya mkopo kwa mtu binafsi na kampuni. Maelezo ya kina yanapatikana katika tovuti ya Wizara www.mifugouvuvi.go.tz, Ofisi za Uvuvi Halmashauri husika na Ofisi za Wizara zinazoshughulika na masuala ya Uvuvi.

Maombi yote yaidhinishwe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na kutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi **kabla ya tarehe 29 Januari, 2024** kupitia anuani ifuatayo;

KATIBU MKUU
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
S.L.P 2847
40487-DODOMA
Simu: +255 26 23 22613
Baruapepe: ps@uvuvi.go.tz

ORD00016048

nilikuta mtoto amelala aki- watoto kuchomwa moto au ruhusa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

# TANGAZO KWA UMMA

## MIKOPO YA PEMBEJEO ZA UFUGAJI SAMAKI KWA VIZIMBA AWAMU YA PILI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inakaribisha maombi ya mkopo wa masharti nafuu. Mkopo huo unalenga kutoa pembejeo za ufugaji samaki kwa vizimba kibiashara katika Ziwa Victoria. Mkopo utajumuisha vizimba vya mviringo vya plastiki na chuma vyenye kipenyo cha mita 6, 8 na 10; vifaranga vya samaki sato; na chakula cha samaki. Walengwa ni vyama vya ushirika/vikundi, makampuni na watu binafsi wanaokidhi vigezo.

Maombi yaambatanishwe na andiko la biashara pamoja na muhtasari wa kikao ulioridhia kukopa na ukomo wa madeni kwa vyama vya ushirika; barua ya dhamana kutoka halmashauri husika kwa vikundi; na dhamana ya mkopo kwa mtu binafsi na kampuni. Maelezo ya kina yanapatikana katika tovuti ya Wizara www.mifugouvuvi.go.tz, Ofisi za Uvuvi Halmashauri husika na Ofisi za Wizara zinazoshughulika na masuala ya Uvuvi.

Maombi yote yaidhinishwe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na kutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kabla ya tarehe 29 Januari, 2024 kupitia anuani ifuatayo;

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**
**S.L.P 2847**
**40487-DODOMA**
**Simu: +255 26 23 22613**
**Baruapepe: ps@uvuvi.go.tz**

177330

217722802

CamScanner

and communal land holders and users, both women and men, in specific re-

administration system.

The project, if well executed, will offer

TURN TO PAGE 2

# Illegal fishing: Minister removes acting director

## *Fishermen extensively use dynamite, a major threat to small-scale fisheries through degradation of coral reefs and other critical habitats and multiplying zones for fish*

**By Guardian Reporter**

FAILURE to come up with bold strategies to stop illegal fishing across the country has led to the suspension from office of the Fisheries director Stephen Lukanga.

Abdallah Ulega, the Livestock and Fisheries minister announced the move to suspend the director yesterday in Dar es Salaam when handing over eleven fishing boats worth 1.85bn/- on loan to fishermen in Dar es Salaam Region.

The loan was provided by the Tanzania Agricultural Development Bank (TADB), he said, opting to suspend the acting director after hearing complaints from fishing sector stakeholders.

They talked of escalation of illegal fishing activities in the coastal zone, especially in Dar es Salaam, about which the minister had handed a one month ultimatum to the director to come up with bold strategies to stop illegal fishing countrywide

Visiting the Lumumba market in Mwanza last month, the minister asked the acting director to issue such strategies, explaining that illegal fishing has for a while been an obstacle to the sector's development.

The minister said the director didn't heed the public directive, thus his position will be occupied by Prof Mohammed Sheikh, the ministerial director for research, training and extension.

Earlier in July, a police report indicated that the city coastline leads in illegal fishing activities using explosives, putting in peril blue economy strategies taken up

TURN TO PAGE 2

CamScanner